

Haya ni baadhi ya mambo au masuala ambayo yanazungumziwa na kuelezewa ndani ya kitabu hiki kwa ufupi (summary).

Kitabu hiki ni maalumu kwa wanafunzi wa elimu ya juu, **lengo** lake kuu ni kutoa mwanga wa namna gani wanapohitimu au wanapokuwa katika masomo wanapaswa kuijandaa pindi watakapoingia katika soko la ajira.

Pia kinawafaa wahitimu na waliopo makazini kwa sababu kimetoa taarifa za shughuli mbalimbali kama vile ujasiriamali na weledi.

Katika kitabu hiki maelezo yatakuwa ya kina lakini katika namna ambayo haitakuchosha kukisoma na kuweza kukumbuka.

Kila kitu hakiwezi kuwa ndani ya kitabu hiki lakini kwa kadiri iwezekanavyo kitatoa mwangaza ambao unajenga msingi wa kuweza kukabiliana na kuweza kuongeza au kujiongeza ili kufikia mafanikio.

Kitabu hiki kinakwenda kujaribu kuziba ombwe (utupu) la mwongozo, jambo ambalo kwa bahati mbaya sehemu kubwa lipo kuanzia katika ngazi za familia mpaka katika taasisi za elimu juu ya masuala ya taaluma na kazi.

Ombwe hili likiwa na sababu mbalimbali za kihistoria, kwa mfano baada ya uhuru miaka ya awali wasomi

walikuwa wachache hivyo kazi za ofisini zilipatikana kirahisi kwa waliokuwa na elimu.

## **SOKO LA AJIRA**

Hali ya upatikanaji wa ajira inatofautiana nchi moja hadi nyingine, mpaka wakati huu kitabu kinavyoandikwa hali ya ukosefu wa ajira duniani ni asilimia 5.2 kwa mwaka 2024 kwa mujibu wa shirika la kazi duniani, ILO (International Labour Organization).

Kufikia mwaka 2021 karibia wanafunzi elfu hamsini na nane walihitimu katika vyuo vikuu vya Tanzania.

Mwaka 2024 kuna zaidi ya wanafunzi laki mbili na elfu sita (206,000) wanaendelea na masomo katika vyuo mbali mbali Tanzania.

Kinachotokea ni kuwa uwezo wa serikali na sekta binafsi kuweza kutengeneza ajira rasmi haujaweza kuwapokea kwa idadi kubwa wahitimu hao makazini.

## **KUJIAJIRI NA KUAJIRIWA**

### **Je niajiriwe au nijiajiri?**

Kujiajiri au kuajiriwa ni matokeo ya utashi na malengo ya mtu. Kuna watu wanaopenda kujiajiri na wanaopenda kuajiriwa. Lakini yote yanategemea pia uwezo binafsi wa mtu.

## **KAZI NA TAALUMA**

### **Umuhimu wa kujiimarisha katika mbinu au fani (skills)**

Kujiimarisha katika fani ni kujenga usoefu wa kutosha katika fani husika,kujihuisha(update) katika fani husika kwa kujifunza na kufanya kazi njia mpya katika fani husika.

Zama na mabadiliko mbalimbali yanatokea kila mara hivyo hatuna budi (imetupasa) kuendana na wakati.

### **KUJENGA MTANDAO (NETWORK)**

Mtandao wa watu wa taaluma na fani mbalimbali ambazo zipo katika mstari wako wa utendaji au wa unayoyatarajia ni nyenzo muhimu katika kukusogezza na kukufikisha unapohitaji kufika.

Kuna njia kadhaa wa kadhaa za kujenga mtandao na kwa bahati nzuri katika zama za sasa unaweza kuwa na mtandao katika kurasa za kijamii ukiachilia suala kufahamiana ana kwa ana.

## **MAKOSA KADHAA YA WAHITIMU**

- ❖ Kutotafuta mwongozo

Mwongozo ni mgumu kupatikana na wakati mwingine mchakato wake unachosha na kuboa, na ndio maana kitabu hiki kinafanya kazi ya kuziba ombwe au uwazi huo.

Wahitimu wengi hawatafuti mwongozo au pengine hawajui namna ya kutafuta mwongozo, kabla ya kufanya jambololote inashauriwa kufanya walau dodoso za awali kuweza kujua mambo kadhaa ya jambo unalotaka kuliendea.

## **UJASIRIAMALI (Entrepreneurship)**

### **Ujasiriamali ni nini?**

**Ujasiriamali** ni shughuli ya kujiajiri, hivyo basi ni vyema tukapitia kidogo kuhusu faida na hasara za kujiajiri, ili uweze kujianaa na kujifunza kukabiliana nazo.

### **FAIDA NA HASARA ZA KUJIAJIRI**

Kujiajiri kuna manufaa mengi ikiwa ni pamoja na yafuatayo;

- i. **Mnyumbuliko;** faida ya kujiajiri ni pamoja na mnyumbuliko (flexibility), yani uhuru wa kuweza kufanya shughuli mbalimbali kwa wakati tofauti na kwa uhuru.

## **Sifa kuu za mjasirimali**

- **Kujitoa;** mjasiriamali ni mtu ambaye anatakiwa kujitoa (commit) na kujituma katika shughuli ya kiuchumi.  
Kuwa na uwezo wa kulifanya jambo hilo kwa kujituma na kwa mwendelezo.
- **Hisia chanya;** mjasiriamali unapaswa kuwa na hisia chanya, na uwezo wa kubakia hivyo hata katika nyakati ngumu.

Hii itakufanya hata katika nyakati ngumu